

USHIRIKI WA MTOTO:

- Mara zote jitahidi kumshirikisha mtoto katika malezi yake na shughuli nyingine zinazomhusu (mfano kumuambia anyanyue mkono/mguu wakati ukimbadilisha).
- Kwa mtazamo chanya, saidia jitihada/juhudi za mtoto katika kushiriki.
- Mruhusu mtoto kutatua changamoto zake kadri iwezekanavyo (mfano anapotaka kugeuka: kugeukia kulalia tumbo badala ya mgongo). Msaidie tu pale inapobidi!



UMAKINI TIMILIFU:

- Mpatie mtoto usikivu/umakini uliokamilika hata kama ni kwa muda mfupi.
- Kuwa muangalifu na hali ya hisia za mtoto wakati wa kufanya shughuli na mtoto.
- Kutana na mtoto ukiwa na umakini, utulivu na uzingativu.

MUANDAE MTOTO:

- Zungumza na mtoto kabla ya kumfanyia jambo mf kumbeba.
- Mtazame mtoto machoni kabla ya kufanyia jambo kama kumbeba.
- Kuwa muangalifu na mapokeo ya mtoto.
- Mbebe mtoto pale unapohisi aekutambua.





ZUNGUMZA NA MTOTO:

- Elezea kile utakachofanya (mfano: Ndio, sasa umeniona, nitakubeba!).
- Tumia kila shughuli inayowezekana, pamoja na zile za kumjali mtoto kama fursa ya kuwasiliana kuzungumza na kumjibu mtoto.
- Pokea/itikia kwa kujali jitihada za mawasiliano ya maneno na yasio ya maneno.



MAELEZO KWA AJILI YA MAWASILIANO

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:

**KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE
SIMU:**

**0754 844 777
0714 157 837**

MHUSIKA:



IRENTE CHILDREN'S HOME

© 2019 Prof. Dr. Ulrike Lütke,
Leibniz Universität Hannover
– All Rights Reserved –

ulrike.luedtke@ifs.uni-hannover.de



Niedersächsisches Ministerium
für Soziales, Gesundheit
und Gleichstellung

Kipeperushi hiki kimetengenezwa kwa msaada wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Afya na Fursa Sawa ya Jimbo la Lower Saxony, Ujerumani

MAFUNZO YA MALEZI YA AWALI NA MAKUZI YA MATAMSHI NA LUGHA KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE, FEB 2018 – SEP 2019



MALEZI YANAYOMJALI MTOTO

Tunawashukuru washiriki wote wa Mafunzo kwa kutunga maudhui na kupigapicha mbalimbali zilizomo kwenye kipeperushi hiki.

Kwa sababu za kimaadili, tunadiriki kutoonyesha sura za watoto walioko kwenye picha.